

# Amerika yasema ina imani nchi za Mreno zitakua huru

**A**MERIKA inayo matumaini kwamba makubaliano ya mazungumzo yaliyokwisha fanywa, yanaweza kufuatwa ili kuwapa watu wa Makoloni ya Mreno katika Afrika nafasi ya kushiriki katika hatua za haki ya kujichagulia kile wanachokitaka.

Bw. Adlal E. Stevenson, Balozi wa Amerika kwenye Umoja wa Mataifa alieleza maoni yake hayo Jumatano baada ya mkutano wa mataifa 11 ya Baraza la Ulinzi, yalipopitisha azimio la kuhimiza Ureno ichukue hatua maalum katika nchi zao, pamoja na kutambua haki za watu kujichagulia kile wanachokitenda.

## Zana za vita

Katika hotuba yake kwenye baraza la Jumuiya la Madola, Balozi Stevenson alieleza wazi siasa ya Amerika kuhusu mambo ya zana za vita, alisema; "Azimio hilo pia limezitaka nchi zilizo wanachama wa baraza hilo kuacha kuipa

Ureno silaha na zana za vita kwa ajili ya matumizi yake kwenye Makoloni yake katika Afrika. Amerika inaona kuwa utoaji wa silaha kwa Ureno kwa matumizi mengine ya aina yoyote katika makoloni yake unaweza pia kuongeza hofu na hatari.

Kwa kufikiria pia mambo hayo akilini, Amerika kwa muja mrefu sasa imekuwa ikifuata siasa ya kutoipa Ureno silaha kwa matumizi katika Makoloni yake hayo. Na katika shabaha hii hili tunakatazwa nia kutuma silaha moja kwa moja katika Makoloni ya Mreno. Amerika itazidi kushikilia juu ya siasa hii.

Tunaamin, alitamka kwamba nchi nyingine zitafuata mfano huu kuzuia mambo ya aina hiyo ambayo yanaweza tu kuongeza hofu na kuzidisha hali ya wasi wasi katika sehemu hizo, na kwamba mataifa

hayo yatashirikiana kwa dhiti kuona kuwa ufumbuzi unapatikana kwa njia za amani."

Azimio hilo ina mabadiliko fulani yaliyopendekezwa na nchi ya Venezuela, baada ya kutolewa na Ghana, Morocco na Philippines hapo awali.

Kura zilipopigwa katika baraza hilo, Themanini zililikubali, na hakuwa na aliyepinga, lakini mataifa matatu hayakupiga kura.

## Haikupiga kura

Bw. Stevenson alisema kuwa Amerika haikupiga kura kwa kwamba azimio hili lilifanywa muda kwa sababu 'batumaini drafti katika njia hasa ya kuweza maafikiano na ufumbuzi wa tatizo hilo. Sote tunatarajia ufumbuzi wa tatizo hilo kwa haraka." Aliliaambiata baraza.

"Wakati Amerika haiwezi kukubaliana na baadhi ya mapendekezo kwenye azimio hilo, tunakubaliana na mengi sana kwenye azimio hilo na kwamba tangu awali Jamburi yetu inaunga mkono shabaha za watu kuchagua kile wanachokitaka".